

JAMHURI YA MUUNGANO WA  
TANZANIA



WIZARA YA KILIMO

MFUKO WA PEMBEJEO  
(AGITF)



### 3. MIKOPO KWA TAASISI ZA FEDHA

Mkopo huu ni maalum kwa Taasisi za Kifedha zinazotoa mikopo kwa wakulima ili kuwafikia wakulima wengi zaidi.

Sifa za Mikopo kwa Taasisi za Fedha

- Riba ya hadi asilimia tano (5%) kwa mwaka
- Muda wa rehema hadi miezi sita (6)



### 2. MKOPO WA MKULIMA

Mkopo huu ni kwa wakulima binafsi, Vikundi, Kampuni zilizosajiliwa, Vyama vya Ushirika (SACCOS na AMCOS) zinazojihusisha na kilimo.

Sifa za Mkopo wa Mkulima

- Riba ya Mkopo ni asilimia saba (7%) kwa mwaka
- Muda wa rehema (*grace period*) hadi miezi 12 kulingana na aina ya mradi.
- Muda wa kulipa mkopo (*loan tenure*) hadi miezi 36 kulingana na aina ya mradi.
- Taratibu za marejesho (*repayment frequency*) inaweza kuwa kwa mwezi, miezi mitatu, miezi sita, kwa mwaka mara moja au kwa mkupuo kulingana na aina ya mradi.
- Dhamana za mkopo huu ni pamoja na mradi wenyewe, Mkataba wa kuuza mazao na Hati miliki ya mali isiyohamishika.



### MAWASILIANO

Mkurugenzi Mtendaji, Mfuko wa  
Pembejeo,  
S.L.P 2382, DODOMA

Simu 0262354166

Nukushi/fax 0262350268

Barua Pepe info @agitf.go.tz

Tovuti www.agitf.go.tz

@agitf\_tz agitf mfuko

## UTANGULIZI

Mfuko wa Pembejeo ni Taasisi ya Serikali inayotoa mikopo ya pembejeo za kilimo pamoja na zana za kilimo. Mikopo hiyo inalenga kupanua maeneo ya kilimo na kuongeza Uzalishaji katika sekta ya kilimo.

### 1. DIRA

Kuwa kinara chaguo katika kutoa mikopo ya Pembejeo na zana kwa riba nafuu kwa wakulima wadogo katika kuitikia wito na mahitaji ya maendeleo ya Kilimo Tanzania.

### 2. DHIMA

Kutoa mikopo ya riba nafuu kwa wakulima, wadogo nchini Tanzania ili kuboresha maisha ya kaya pamoja na usalama wa chakula wa Taifa.



## 3. MADHUMUNI

Kupanua maeneo ya kilimo na kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo na kuongeza ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo

## 4. WALENGWA.

- Wakulima binafsi;
- Vikundi vilivyosajiliwa; vinavyojihusisha na shughuli za kilimo;
- Kampuni zilizosajiliwa zinazojihusisha na shughuli za kilimo;
- Vyama vya Ushirika (SACCOS na AMCOS) na
- Taasisi za Fedha.

## 5. MAENEO YANAYO GHARAMIWA NA MIKOPO YA MFUKO WA PEMBEJEO

- Kilimo cha umwagiliaji;
- Uongezaji thamani wa mazao ya kilimo na mifugo;
- Uhifadhi wa mazao ya kilimo;
- Kilimo cha mazao ya muda mfupi (Mbogamboga, Viazi, Matunda, Mahindi Mabichi, n.k.);
- Pembejeo za kilimo;
- Gharama za uendeshaji wa shughuli za kilimo na
- Zana za kilimo (matrekta ya mikono na mashine za kilimo).

## AINA ZA MIKOPO NA TARATIBU ZAKE

### 1. MKOPO WA MKULIMA NAFUU

Huu ni mkopo kwa Vijana na Wanawake wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 40 wanaojihusisha na shughuli za kilimo.

#### Sifa za Mkopo wa Mkulima Nafuu

- Riba Nafuu ya 4.5% kwa mwaka.
- Muda wa rehema (grace period) hadi miezi 6 kulingana na aina ya mradi.
- Muda wa kulipa mkopo (loan tenure) hadi miezi 36 kulingana na aina ya mradi.
- Taratibu za marejesho (repayment frequency) inaweza kuwa kwa mwezi, miezi mitatu, miezi sita, kwa mwaka mara moja au kwa mkupuo kulingana na aina ya mradi.

